




Funded by  
the European Union




*Mradi unasa idia vijiji 31 kuboresha ardhi na utawala bora wa rasilimali asilia*

Mradi huu unatekelezwa kwa ubia kati ya Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Mradi huu unafadhiliwa na Umoja wa nchi za Ulaya kwa kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka 2013 hadi 2017.

## MRADI UNATEKELEZWA KWENYE VIJI VIPI

Mradi unatekelezwa kwenye vijiji 31 vilivyo kando kando ya Misitu wa Hifadhi wa Kanga na Hifadhi ya Asilia ya Mkingu. Misitu ya Milima ya Nguru Kusini ni chanzo muhimu cha maji Tanzania na ni sehemu ambapo kuna wanyama na mimea ya kipekee.



## LENKO KUU LA MRADI

Mradi unalenga kupunguza umasikini na kuboresha shughuli za kiuchumi kwa jamii zinazoishi kando kando ya misitu na zinazotegemea rasilimali zinazotokana na misitu iliyoko kwenye wilaya ya Mvomero Morogoro.

## LENKO MAHUSUSI LA MRADI

Kuimarisha usimamizi shirkishi wa misitu na kuwa na ukuwaji wa uchumi endelevu kwa jamii zinazo zunguka misitu ya Nguru kusini.



**AFYA NZURI NI MSINGI ILINDE FAMILIA YAKO NA VIRUSI VYA UKIMWI**

Kwa mawasiliano zaidi:

Mkurugenzi Mtendaji, TFCG, S.L.P 23410, Dar es Salaam, Simu: +255 22 2669007  
Mkurugenzi Mtendaji, MJUMITA, S.L.P 21522, Dar es Salaam, Simu: +255 22 2669007  
Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, S.L.P 663 Morogoro  
Mtendaji Mkuu, Wakala wa huduma za Misitu Tanzania, S.L.P 40832, Dar es Salaam  
Mvomero: +255 23 2613223; Wakala wa huduma za misitu: +255 22 2864249

**OFISI YA MRADI IPO MADIZINI B NYUMA YA KISII GUEST HOUSE KILOMITA 1.3 KUTOKA VIBAONI.**

# MRADI WA KUONGEZA THAMANI YA MISITU YA TAO LA MASHARIKI, WILAYA YA MVOMERO, MOROGORO

## JINSI GANI WANAJAMII WATANUFAIKA NA MRADI HUU

### 1. Mipango ya matumizi bora ya ardhi za vijiji

Mpango utawawezesha wanakijiji kufanya maamuzi ya ardhi yao kwa njia shirkishi na kuzingatia utaalamu na sheria za nchi. Mpango huu unawawezesha wakijiji kupata manufaa kama:

- Kupunguza na kutatua migogoro ya ardhi inayotokana na matumizi ya ardhi (wafugaji na Wakulima).
- Kijiji kitapata cheti cha ardhi ya kijiji.
- Mwanakijiji mmoja mmoja ataweza kupata hati ya kimila ya kumiliki ardhi.




*Wananchi wote wanatiwa moyo wakushiriki kwenye zoezi la maandalizi ya matumizi bora ya ardhi*

### 2. Wanakijiji watapata fursa ya kusimamia misitu ilio ndani ya mipaka ya kijiji

Wanakijiji watajengewa uwezo wa kutenga na kusimamia misitu iliyopo ndani ya kijiji chao na kuweza kuandaa mpango wa usimamizi wa misitu hiyo n, kama wataisimamia vizuri, wataweza kupata faida nyingi ikiwemo:

- Uvunaji wa mazao timbao (mfano mbao, nguzo, n.k) na yasiyo timbao (matunda, dawa n.k) kwa njia endelevu.
- Malipo yatokanayo na MKUHUMI kama watapunguza ufye kaji na uharibifu wa misitu na taratibu kukamilika.
- Kuepukana na ukame na kuongezaka kwa vyanzo vya maji, n.k.



*Misitu ya Milima ya Nguru Kusini ni chanzo muhimu cha maji kwa jamii inayoishi Wilayani Mvomero*

3. Wanakijiji watapa fursa ya kusimamia Misitu ya serikali kuu wakishirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania



*Misitu ya Milima ya Nguru Kusini ni nyumbani mwa wanyama na mimea adimu ambayo haipatikani mahali pengine popote duniani.*

Mfumo huu wa usimamizi wa pamoja wa msitu unatoa fursa kwa jamii kuingia mkataba na serikali kuu kuweza kusimamia misitu kwa pamoja ili kuboresha misitu na pia wanajamii kunufaika kutokana na misitu hii. Wanajamii watafaidika na mgawanyo wa mapato kutokana na utaratibu huu, hivyo kupata fedha kwa ajili ya maendeleo ya kijiji na jamii kwa ujumla.

### 4. Miradi/shughuli mbadala za kujiongezea kipato zitaibuliwa.



*Mradi utawasidia wakulima kuweza kutumia mbinu bora za kilimo pamoja na kilimo hifadhi*

Mradi utawawezesha wananchi kuanzisha na kuendeleza shughuli mbadala za kujiongezea kipato ambazo ni rafiki wa mazingira. Baadhi ya shughuli ambazo wanajamii wataweza kunufaika nazo ni kama:

- Ufugaji wa kisasa wa nyuki.
- Vikundi vya kuweka na kukopa (Hisa).
- Vitalu vya miti mashule.
- Mafunzo ya Kilimo hifadhi.
- Kilimo cha uyoga.
- Biashara ya hewa ukaa.
- Matumizi ya majiko banifu.



*Mradi unatoa mafunzo kwa wanawake na wanaume iliwawaeza kupata kipato kutokana na kuuza asali na nta*



Tanzania Forest  
Conservation Group  
Shirkika la Kuhifadhi  
Misitu ya Asili Tanzania

